# HALI YA HAKI ZA BINADAMU DUNIANI

APRILI 2024



AMNESTY INTERNATIONAL

# AMNESTY INTERNATIONAL

Amnesty International ni vuguvugu la watu milioni 10 ambalo linahamasisha ubinadamu wa kila mmoja wetu na kuendesha kampeni ya kuleta mabadiliko ili kwamba sisi sote tuweze kunufaika na haki zetu za kibinadamu. Dira yetu ni kuona kwamba waliopo madarakani wanatimiza ahadi zao, wanaheshimu sheria za kimataifa na wanaweza kuwajibishwa. Hatufungamani na serikali yoyote, itikadi ya kisiasa, maslahi ya kiuchumi au dini na kwa sehemu kubwa tunafadhiliwa na wanachama wetu na michango binafsi. Tunaamini kwamba kwa kufanya kazi kwa mshikamano na upendo na watu kila mahali tunaweza kubadilisha jamii zetu kuwa bora zaidi.

Amnesty International haina upendeleo. Hatutoi msimamo wetu kuhusu masuala ya mamlaka ya nchi, migogoro ya mipaka kati ya nchi na nchi au makubaliano ya kisiasa na kisheria ambayo yanaweza kufanyika ili kutekeleza haki ya watu kujiamulia hatima yao wenyewe. Kwa kuzingatia hilo na nia yetu ya kuangazia suala la uwajibikaji wa serikali, tunatoa maelezo yetu kuhusu haki za binadamu duniani kulingana na idara za dola zinazowajibika kwa hali ya haki za binadamu katika nchi husika.

Imechapishwa kwa mara ya kwanza mwaka wa 2024 na Amnesty International Ltd
Peter Benenson House
1 Easton Street
London WC1X 0DW
Uingereza

© Amnesty International 2024

Fahirisi: POL 10/7200/2024
ISBN: 978-0-86210-509-9
Lugha ya Asili: Kiingereza
Isipokuwa kama imebainishwa vinginevyo, maudhui katika chapisho hili yapo chini ya leseni ya CreativeCommons (kunukuu, matumizi yasiyo ya kibiashara, kutofanyiwa mikataba ya kifedha inayohusisha pande mbili au zaidi, kimataifa 4.0).
https://creativecommons.org/licenses/by-nc-nd/4.0/legalcode
Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea ukurasa wetu wa kutoa idhini kwenye tovuti yetu:
www.amnesty.org

Ripoti hii inazungumzia maendeleo muhimu ya haki za binadamu katika ngazi ya taifa na kanda katika kipindi cha mwaka 2023, pamoja na kutoa uchambuzi wa kimataifa wa changamoto kubwa za haki za binadamu zilizopo kwa sasa. Inahusisha maelezo kuhusu nchi au mamlaka za ardhi ambazo hali yake ya haki za binadamu imechunguzwa na Amnesty International katika kipindi cha mwaka 2023.

Kutokuwemo kwa nchi au mamlaka fulani ya ardhi haina maana kwamba katika sehemu hiyo hapakuwepo ukiukwaji wa haki za binadamu ulioipa wasiwasi Amnesty International katika mwaka husika. Vivyo hivyo, urefu wa taarifa kuhusu nchi fulani si msingi wa kulinganisha ukubwa na uzito wa wasiwasi wa Amnesty International katika sehemu hiyo. Ripoti hii haigusii kwa kina matumizi ya adhabu ya kifo kwa kuwa Amnesty International inatoa taarifa tofauti ya kimataifa kila mwaka kuhusu adhabu ya kifo na unyongaji.

# HALI YA HAKI ZA BINADAMU DUNIANI

## APRILI 2024

# YALIYOMO


**MUHTASARI WA KANDA YA AFRIKA** **5**
MASHAMBULIZI HARAMU NA MAUAJI 5
MAPIGANO YANAYOHUSISHA UKATILI WA KINGONO NA KIJINSIA 6
KUZIMA MAWAZO TOFAUTI 6
HAKI ZA KIUCHUMI NA KIJAMII 9
HAKI ZA WATU WALIOPOTEZA MAKAZI NCHINI MWAO, WAKIMBIZI NA WAHAMAJI 10
UBAGUZI 11
HAKI YA KUWA NA MAZINGIRA SALAMA 12
HAKI YA KUPATA UKWELI, HAKI NA FIDIA 12

**KENYA** **14**
MAUAJI YA MAKUSUDI NJE YA UTARATIBU WA SHERIA NA KUPOTEZWA KWA NGUVU 14
UHURU WA KUJIELEZA NA KUKUSANYIKA 15
HAKI YA KUISHI 15
HAKI YA KUPATA UKWELI, HAKI NA FIDIA 15
HAKI ZA WAPENZI WA JINSIA MOJA (LGBTI) 15
HAKI ZA KIUCHUMI NA KIJAMII 16
HAKI YA AFYA 16
HAKI YA KUWA NA MAZINGIRA SALAMA 16
HAKI YA KUWA NA FARAGHA 17
ADHABU YA KIFO 17

**TANZANIA** **18**
UHURU WA KUJIELEZA, KUJUMUIKA NA KUKUSANYIKA 18
KUHAMISHWA KWA NGUVU 19
HAKI YA KUWA NA MAZINGIRA SALAMA 19
HAKI YA KUPATA UKWELI, HAKI NA FIDIA 20
HAKI ZA WANAWAKE NA WASICHANA 20
HAKI ZA WAPENZI WA JINSIA MOJA (LGBTI) 20

# MUHTASARI WA KANDA YA AFRIKA

**Kuzuka upya kwa machafuko huko Sudan kunaangazia namna ambavyo raia wanaojikuta katika mapigano ya silaha wanavyopata mateso makubwa katika kanda yote, na kudharau kabisa sheria ya kimataifa ya ubinadamu kunakofanywa na pande zote zinazohusika katika migogoro. Ripoti za kuuawa raia kwa wingi zilikuwa nyingi na za kutisha, hasa ikizingatiwa ukubwa wa mashambulio ya kiholela na yanayolenga makundi maalum. Ukatili wa kijinsia uliendelea kuwa moja ya matukio katika migogoro ya mapigano ya silaha za moto.**

**Kukosoa serikali iliendelea kuwa jambo la hatari katika nchi nyingi za Afrika. Kuwashambulia vikali waliopinga matumizi mabaya ya serikali, kushindwa kutekeleza wajibu, au tuhuma za rushwa ni jambo lilionea kote na hasa wakilengwa waandishi wa habari, watetezi wa haki za binadamu, wahamasishaji na viongozi na wanachama wa vyama vya upinzani. Kuuawa kwa mtetezi mashuhuri wa haki za binadamu wa Eswatini, Thulani Maseko na mwandishi wa habari wa Cameroon, Martinez Zongo, na kifo cha kutatanisha cha mwandishi wa habari za uchunguzi wa Rwanda, John Williams Ntwali, katika wiki moja mwezi Januari, ilikuwa kipindi cha giza katika harakati za utetezi wa haki za binadamu.**

**Sababu mbalimbali, ikiwemo mfumuko wa bei, rushwa, mabadiliko ya tabianchi na migogoro, zilitengeneza hali ya maisha isiyovumilika. Mamilioni ya watu walishindwa kupata haki za msingi za kiuchumi na kijamii. Nchi nyingi ziliathirika kwa kiwango kinachotofautiana kwa ongezeko kubwa la mfumuko wa bei za vyakula, na ukosekanaji wa usalama wa chakula ulifikia viwango vya kutisha.**

**Mapigano ya silaha za moto yasiyokoma na hali mbaya ya hewa, ilifanya mamilioni ya watu kukimbia makazi yao, na bado nchi kadhaa zilipuuzia wajibu wao wa kuwapa ulinzi wakimbizi na watu waliokuwa wakitafuta hifadhi.**

**Ubaguzi wa kijinsia na ukatili dhidi ya wanawake na wasichana uliendelea kuwa mkubwa, wakati mashambulizi dhidi ya wapenzi wa jinsia moja na ukiukwaji wa haki za binadamu za wapenzi wa jinsia moja (LGBTI) uliongezeka katika kanda yote.**

**Kwa sehemu kubwa serikali za Afrika ziliendelea kukaidi wito wa kuzitaka kuchukua hatua dhidi ya kutojali sheria, na hivyo kufanya jambo hilo kushamiri, likichochea mwendelezo wa migogoro na ukatili, na kutozingatia utawala wa sheria. Serikali nyingi zilidhoofisha mipango ya upatikanaji haki na uwajibikaji au kuvuruga wazi wazi uchunguzi wa kimataifa wa rekodi zake za haki za binadamu.**

## MASHAMBULIZI HARAMU NA MAUAJI

Migogoro iliyohusisha mapigano ya silaha za moto iliendelea kuwa na madhara makubwa kwa raia katika nchi za Burkina Faso, Cameroon, Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Mali, Nigeria, Somalia, Sudan na kwingineko. Kama hawakuwa wamelengwa kwa makusudi, ikiwemo mashambulizi ya kimbari, raia ndiyo walioathirika zaidi na mashambukizi ya kiholela, ambayo wakati mwingine yalikuwa kwa njia ya mashambulizi ya angani, roketi na makombora na silaha nyingine za milipuko zenye madhara kwenye maeneo makubwa. Baadhi ya mashambulizi hayo yalikuwa kabisa uhalifu wa kivita.

Nchini Sudan, zaidi ya watu 12,000 waliuawa katika mapigano yaliyozuka kati ya Majeshi ya Serikali ya Sudan na Majeshi ya Mwitikio wa Haraka ya Sudan (RSF). Mashambulio yaliyolenga maeneo maalum nchini humo, ikiwemo mji mkuu, Khartoum, lakini hasa Darfur Magharibi, yaliua na kujeruhi raia, sawa na silaha za milipuko iliyorushwa na SAF na RSF kutokea katika maeneo ya wakazi wengi.

Nchini Burkina Faso, wanachama wa kikundi cha mapigano cha *Ansaroul Islam* waliua raia takribani 60 katika mji wa Partiaga mwezi Februari; miezi sita baadaye waliua watu 22 katika mji

wa Nohao. Majeshi ya serikali yalilenga raia. Katika tukio moja, askari, wakiwa na wanamgambo wa Kulinda Nchi, waliua raia takribani 147 katika kijiji cha Karma. Huko DRC, makundi yenye silaha yaliua watu takribani 4,000 na kujeruhi maelfu. Katika mkoa wa Nord-Kivu, wapiganaji wa kikundi cha *Allied Democratic Forces* waliua watu 23 kwa mapanga. Katika mkoa wa Ituri, watu takribani 46, nusu yao wakiwa watoto, waliuawa kwa risasi na kukatwa mapanga katika usiku mmoja na wapiganaji wa *Cooperative for the Development of the Congo.* Nchini Mali, mashambulizi yaliyofanywa na *Islamic State* huko Sahel katika vijiji vya Gaina na Boyna, Mkoa wa Gao, yaliua watu 17. Miezi miwili baadaye, shambulizi la wanachama wa *Group for the Support of Islam and Muslims* katika vijiji vya Bodio na Yarou mkoa wa Bandiagara, lilisababisha vifo vya raia 37.

Shambulio la ndege lililofanywa na jeshi la anga la Nigeria liliua raia 21 katika jimbo la Niger, wakati mapigano kati ya majeshi ya usalama ya Somaliland na wapiganaji wa silaha za moto yalisababisha vifo vya raia 36, nchini Somalia, hasa kutokana na upigaji makombora kiholela katika mji wa Las Anod uliofanywa na majeshi ya usalama ya Somaliland.

**Mahasimu katika mapigano ya silaha lazima walinde raia kwa kutofanya mashambulizi kiholela na kulenga makundi maalum ya raia na miundombinu ya kiraia.**

## MAPIGANO YANAYOHUSISHA UKATILI WA KINGONO NA KIJINSIA

Ukatili wa kingono na kijinsia ulioenea mahali kote, ikiwemo ubakaji, ubakaji wa kundi (ubakaji wa mtungo), utoroshaji na utumikishwaji kingono uliendelea, na wahanga wengi hawakuwa na uwezo wa kupata msaada wa matibabu muhimu na usaidizi wa kijamii na kisaikolojia. Askari wa Jeshi la Ulinzi la Eritrea waliwashikilia wanawake takribani 15 kwa karibu miezi mitatu kwenye kambi ya kijeshi katika jimbo la Tigray, Ethiopia, wakiwabaka kwa kurudia. Nchini Burkina Faso, wanaodaiwa kuwa wanachama wa *Ansaroul Islam* waliteka wanawake 66, wasichana na watoto wachanga kwenye kijiji cha Liki katika mkoa wa Sahel. Waliachiwa huru siku nne baadaye kwenye kizuizi cha mji wa Tougouri. Wapiganaji wa *Boko Harem* waliteka wanawake 40 katika eneo la serikali ya mtaa ya Mafa katika jimbo la Borno, Nigeria.

Nchini CAR, Umoja wa Mataifa ulitoa tamko kwamba ulikuwa na ushahidi wa ubakaji, ukiwatuhumu askari 11 wa kulinda amani kutoka Tanzania. Nchini DRC, zaidi ya matukio 38,000 ya ukatili wa kingono yaliripotiwa katika mkoa wa Nord-Kivu pekee katika robo ya kwanza ya mwaka 2023. Nchini Mali, Umoja wa Mataifa uliorodhesha matukio 51 ya ukatili wa kingono katika migogoro, dhidi ya wanawake na wasichana katika kipindi hicho. Nchini Sudan, makumi ya wanawake na wasichana walifanyiwa ukatili wa kingono, ikiwemo kubakwa, na wanachama wa pande zinazopigana, hasa kutoka RSF na wanamgambo walio washirika wake. Katika tukio moja, askari wa RSF waliwateka wanawake na wasichana 24, wakiwashikilia kwenye hoteli katika mji wa Nyala kwa siku kadhaa katika mazingira yaliyokuwa sawa na utumwa wa kingono.

**Pande zinazohusika katika mapigano zinapaswa kutoa amri bayana kwa wanachama au majeshi yao, ambazo zinakataza ukatili wa kingono na kijinsia; na serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba wahanga wa ukatili kama huo wanapata matibabu kamili na tiba ya kijamii na kisaikolojia.**

## KUZIMA MAWAZO TOFAUTI

### UHURU WA KUKUSANYIKA KWA AMANI

Katika kanda yote, waandamanaji waliingia mitaani kutoa dukuduku lao kuhusu masuala kadhaa, ikiwemo gharama kubwa za maisha, utawala mbovu na ukiukwaji wa haki za binadamu. Katika matukio mengi, majeshi ya usalama yaliwatawanya waandamanaji kwa kutumia nguvu kubwa kupita kiasi; makumi ya waandamanaji na waangaliaji waliuawa na kujeruhiwa, ikiwemo nchi za Angola, Ethiopia, Kenya, Mali, Msumbiji, Senegal na Somalia. Polisi nchini Kenya waliua watu takribani 57 wakati wa maandamano kati ya mwezi Machi na Julai. Nchini Senegal, watu takribani 29 waliuawa mwezi Juni wakati polisi na watu wenye silaha waliokuwa wamevalia kiraia

walipofyatua risasi za moto kuwatawanya waandamanaji waliokuwa wakifanya vurugu katika mji mkuu, Dakar, na Ziguinchor.

Katika matukio mengine, maandamano yalizuiwa kabla, ikiwemo nchi za Chad, Guinea, Senegal na Sierra Leone. Marufuku ilielekezwa zaidi kwenye mikusanyiko na maandamano yaliyoitishwa na asasi za kiraia au viongozi au vyama vya upinzani. Nchini Chad, maandamano mawili yaliyoandaliwa na vyama vya upinzani yalikuwa kati ya yale yaliyopigwa marufuku na Wizara ya Usalama wa Umma, kimsingi kwa sababu vyama hivyo havikuwa na usajili kisheria na havikuwa vimetimiza masharti ya kuidhinishwa kufanya maandamano. Nchini Guinea, katazo la jumla, dhidi ya mikutano yote ya kisiasa lililowekwa kuanzia Mei 2022, liliendelea kutumika ingawa mikutano kadhaa ya kumuunga mkono mkuu wa nchi iliruhusiwa kuendelea.

## UHURU WA KUJIELEZA

Vitisho dhidi ya haki ya uhuru wa kujieleza viliendelea. Kukosoa sera za serikali, utendaji wake au kutotenda kwake, au kusambaziana habari wazi wazi ambayo ilionekana kama kuichafua serikali kuliambatana na hatari ya kutiwa mbaroni, kuwekwa kizuini bila kuzingatia sheria, au kifo. Thulani Maseko, mtetezi wa haki za binadamu nchini Eswatini, aliuawa nyumbani kwake. Maiti ya mwandishi wa habari Martinez Zogo iliyokuwa imeharibika vibaya ilipatikana siku tano baada ya kutekwa katika viunga vya Jiji la Yaoundé nchini Cameroon. Alikuwa akiandika madai ya tuhuma za rushwa kuhusiana na watu wakubwa serikalini. John Williams Ntwali, mwandishi wa habari za uchunguzi aliyekuwa akiandika masuala yanayohusu haki za binadamu, alikufa katika mazingira ya kutatanisha nchini Rwanda, siku moja baada ya kumwambia mwandishi wa habari mwingine kwamba alikuwa akihofia usalama wake.

Nchini Sudan Kusini, waandishi saba wa habari walitiwa kizuizini bila kuzingatia sheria kwenye mahabusu za Shirika la Usalama wa Taifa katika mji mkuu, Juba, kuhusu video iliyokuwa ikisambaa mtandaoni, ambayo ilidaiwa kumuonesha Rais akijikojolea. Walishikiliwa kwa vipindi mbalimbali vya hadi wiki 10 na kuachiwa bila kufunguliwa mashtaka; mmoja wao alionekana kuwa ameteswa na kwa namna nyingine kufanyiwa ukatili.

Nchini Somalia, mahakama ilimhukumu Abdalle Ahmed Mumin, mwandishi wa habari na katibu mkuu wa Umoja wa Waandishi wa Habari wa Somalia, kwenda jela miezi miwili kwa kukaidi “amri za serikali”. Akiwa tayari amekaa rumande kwa miezi miwili, aliachiwa huru lakini akakamatwa tena wiki moja tu baadaye na kutiwa kizuizini kwa mwezi mwingine. Nchini Tanzania, watu takribani 12 walikamatwa kati ya mwezi Juni na Desemba kwa kukosoa mkataba wa uwekezaji katika bandari kati ya Tanzania na UAE, na waliachiwa bila masharti baada ya siku chache.

Utumiaji wa mahakama kuwanyanyasa wakosoaji wa serikali pia ilikuwa jambo la kawaida. Nchini Burundi, mwandishi wa habari wa kike, Floriane Irangabiye alihukumiwa kwenda jela miaka 10 kwa “kudhalilisha hadhi ya ardhi ya taifa”. Hukumu yake, kutokana na maoni aliyoyatoa kwenye kipindi cha redio, ilikubaliwa na mahakama ya rufaa. Nchini Benin, Virgile Ahouansè, mkurugenzi wa habari wa redio ya mtandaoni, alihukumiwa kifungo cha nje cha miezi 12 kwa kusambaza “habari potofu”. Mwaka 2022, alikuwa amerusha hewani habari ya uchunguzi iliyokuwa na maelezo ya mashahidi ikiwahutumu polisi kufanya mauaji bila ya kuwafikisha watu mahakamani. Nchini Niger, Samira Ibrahim alitiwa hatiani kwa “kutoa maelezo… ya kuvuruga amani ya nchi”, baada ya mwandishi huyo wa kike kudai katika mtandao wa Facebook kuwa Algeria haiitambui serikali ya kijeshi ya Niger.

Waandishi kadhaa wa habari, wanaharakati na watetezi wa haki za binadamu, wakiwemo wa nchi za CAR, Chad, Mali, Tanzania na Togo, walilazimika kukimbilia uhamishoni. Nchini Togo, Ferdinand Ayité na Isidore Kowonou wa gazeti la *L’Alternative* walihukumiwa kwenda jela miaka mitatu na kulipa faini kubwa baada ya kuchapisha makala iliyowatuhumu wafanyakazi wawili wa serikali kwa rushwa. Waliikimbia nchi kuepuka kutumikia hukumu zao. Nchini CAR, mwandishi wa habari aliyeandika kuhusu tuhuma za rushwa katika Bunge aliikimbia nchi, baada ya kupata vitisho kutoka chanzo kisichojulikana. Nchini Mali, mtetezi wa haki za binadamu Aminata Dicko alilazimika kukimbilia uhamishoni baada ya kuelezea ukiukwaji unaofanywa na majeshi ya ulinzi katika maelezo yake kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ambapo baadaye polisi walimwita kwa mahojiano kuhusu tuhuma za uhaini na kashfa.

Katika nchi za Benin, Burkina Faso, Chad, Niger, Togo na kwingineko, mamlaka ziliamuru kusimamishwa kwa muda vyombo vya habari, magazeti au tovuti za habari kwa vipindi tofauti. Zikiwa zinakabiliwa na machafuko ya kijamii au kisiasa, mamlaka huko Ethiopia, Guinea, Mauritania na Senegal zilisitisha kwa muda au kuvuruga upatikanaji wa mtandao. Tume ya Taifa ya Utangazaji ya Nigeria ilivitoza faini vituo 25 kuhusiana na utoaji taarifa zao kuhusu uchaguzi mkuu wa mwaka 2023 kwa madai ya kuvunja kanuni za utangazaji. Mamlaka nyingine zilikwenda mbali zaidi, ikiwemo nchi ya Benin ambapo gazeti la *Gazette du Golfe* lilisimamishwa kwa muda usiojulikana. Nchini Burkina Faso, waandishi wawili wa kigeni walifukuzwa nchini humo na katika nchi ya Niger, gazeti la *L'Évènement* lilifungiwa kwa madai ya kutolipa kodi.

### UHURU WA KUKUSANYIKA

Makatazo makali na yasiyokuwa na sababu kuhusu haki ya kukusanyika yaliongezeka. Vilivyolengwa ni vyama vya upinzani na uwezo wao wa kupanga na kuendesha shughuli zao kwa uhuru ulifinywa. Nchini Burundi, serikali ilisimamisha karibia shughuli zote za chama kikuu cha upinzani, *National Congress for Liberty*. Kufuatia mapinduzi ya kijeshi ya mwezi Julai nchini Niger, jeshi lilipiga marufuku shughuli zote za vyama vya siasa kwa muda usiojulikana. Nchini Uganda, mikutano ya kampeni na shughuli nyingine za chama cha *National Unity Platform* zilipigwa marufuku. Aidha inatia moyo kwamba Rais wa Tanzania alifuta amri ya mwaka 2016 iliyokataza vyama vya siasa kufanya mikutano na shughuli nyingine za kisiasa.

Serikali ziliendelea kutumia sheria kama silaha ya kufinya haki za binadamu, ikiwemo haki ya uhuru wa kukusanyika. Nchini Angola, mswada wa sheria ya asasi za kiraia, ambao kulingana na asasi za kiraia, ungeweza kufinya uhuru wa haki ya kukusanyika na kuipa serikali mamlaka kubwa kuingilia shughuli za asasi hizo, ulipitishwa na Bunge kuwa sheria kamili.

### KUTIWA MBARONI NA KIZUIZINI KIHOLELA, NA UTESAJI NA UONEAJI MWINGINE

Kutiwa mbaroni na kizuizini kiholela uliendelea kuenea kwa sehemu kubwa. Kutiwa mbaroni na kizuizini kiholela, mara nyingi, ilitumika wakati wa kutawanya maandamano uliofanywa na vikosi vya usalama au katika kutekeleza utangazaji wa hali ya dharura. Mwezi Agosti serikali ya Ethiopia ilitangaza hali ya dharura nchi nzima kwa miezi sita, kufuatia mapigano kati ya jeshi na wanamgambo wa Fano katika mkoa wa Amhara. Ilitoa kisingizio cha kuwatia kizuizini mamia ya watu ambao walinyimwa haki ya kupata wanasheria na kupelekwa mahakamani. Nchini Senegal zaidi ya watu 1,000 walikamatwa na kutiwa kizuizini kwa kushiriki katika maandamano, au madai ya kuhusika na chama cha upinzani cha PASTEF.

Katika nchi nyingine, zikiwemo Botswana, Burundi, Niger na Zimbabwe, wanasiasa mashuhuri walikamatwa au kuzuiliwa bila ya kufuata utaratibu wa kisheria. Nchini Botswana, viongozi kadhaa wa chama cha upinzani cha *Botswana Patriotic Front*, na waandishi wa habari wawili, walikamatwa na kuzuiliwa bila ya kufunguliwa mashtaka kwa siku mbili. Kufuatia mapinduzi ya kijeshi Niger, Rais Bazoum na familia yake waliwekwa kizuzini Ikulu. Maafisa wengine kadhaa wa serikali ya zamani na chama tawala walitiwa kizuizini bila ya kufunguliwa mashtaka. Nchini Zimbabwe, Jacob Ngarivhume, kiongozi wa chama cha upinzani cha *Transform Zimbabwe* aliachiwa huru baada ya kukata rufaa miezi minane tangu alipohukumiwa kwenda jela miezi 48 (12 ikiwa kifungo cha nje). Alikuwa amekamatwa Julai 2020 kwa kuongoza na kuandaa maandamano ya kupinga rushwa.

Kutiwa mbaroni na kizuizini kiholela pia ilitajwa kutokea nchi za DRC, Equatorial Guinea, Mali na kwingineko.

Mateso na aina nyingine za kutendewa vibaya yaliendelea kuwa mambo yaliyosababisha hofu kubwa. Vifo vya kutatanisha chini ya ulinzi wa polisi viliripotiwa katika nchi kadhaa, zikiwemo Equatorial Guinea, Lesotho, Mauritania na Nigeria. Nchini Mauritania, mtetezi wa haki za binadamu Souvi Ould Jibril Ould Cheine alikufa baada ya mahojiano katika kituo cha polisi. Uchunguzi wa kidaktari wa mwili wake ulisema kifo chake kilisababishwa na kukosa hewa, jambo lililotofautiana na maelezo ya serikali kwamba alikufa kutokana na mshtuko wa moyo. Mwendesha mashtaka wa serikali aliamuru kukamatwa kwa kamishina na askari polisi waliohusika. Nchini Nigeria, Faiz Abdullahi alikufa chini ya uangalizi wa polisi katika jimbo la Kaduna, baada ya

kuteswa wakati wa mahojiano. Mwanafunzi wa miaka 17 alifia hospitalini baada ya kuteswa wakati wa mahojiano na polisi katika jimbo la Adamawa.

### MAUAJI KINYUME CHA SHERIA NA KUPOTEZWA KWA NGUVU

Katika nchi kadhaa, mauaji kinyume cha sheria na mauaji mengine bila ya kufuata sheria na kupotezwa kwa nguvu yaliendelea kutumika kama njia ya ukandamizaji. Nchini Burkina Faso, watu mashuhuri walitekwa au kukamatwa na kupotezwa kwa nguvu, akiwemo rais wa kitaifa wa umoja wa kuwakilisha maslahi ya wafugaji. Nchini Burundi, taarifa za watu kupotezwa kwa nguvu, hususani wapinzani wa kisiasa, ziliendelea kutolewa, Shirika la Usalama wa Taifa na wanachama wa jumuiya ya vijana ya chama tawala, *Imbonerakure*, walikuwa ndiyo watuhumiwa wakubwa wa uhalifu huo. Nchini Eritrea, hatima na walipo wanachama 11 wa G-15, ambalo ni kundi la wanasiasa wakongwe 15 waliomkosoa hadharani Rais mwaka 2001, iliendelea kutojulikana pamoja na waandishi wa habari 16 waliotuhumiwa kuwa na uhusiano na G-15.

**Serikali lazima zikomeshe mara moja unyanyasaji na udhalilishaji wa waandishi wa habari, watetezi wa haki za binadamu, wanaharakati na wanachama na viongozi wa upinzani; na kumwachia huru bila masharti yoyote mtu yoyote aliye kizuizini bila kufuata sheria; na kuhakikisha uhuru wa vyombo vya habari unaheshimiwa, pamoja na kuruhusu vyombo vya habari kujiendesha kwa uhuru.**

## HAKI ZA KIUCHUMI NA KIJAMII

### HAKI YA KUPATA CHAKULA

Nchi nyingi za Kiafrika zilikuwa kati ya nchi nyingi za duniani zilizoathirika sana na mfumuko mkubwa wa bei za chakula. Idadi ya watu wasiokuwa na usalama wa chakula ilifikia viwango ya kutisha. Shirika la Chakula Duniani (WFP) lilikadiria kwamba hadi kufikia mwezi Februari, asilimia 78 ya raia wa Sierra Leone hawakuwa na usalama wa chakula na asilimia 20 ya kaya hazikuwa na usalama wa chakula kwa kiwango kikubwa sana. Mwezi Desemba, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuratibu Misaada ya Binadamu (OCHA), lilisema kwamba watu milioni 5.83 (asilimia 46 ya idadi ya watu wa Sudan Kusini) walikuwa na kiwango kikubwa cha ukosefu wa usalama wa chakula. Nchini Namibia, ukosefu mkubwa wa usalama wa chakula uliongezeka kwa kiasi kikubwa sana, ukiathiri asilimia 22 ya idadi ya watu wote.

Mabadiliko ya tabianchi na matukio makubwa ya hali ya hewa yaliongeza ukubwa wa tatizo la chakula. Nchini Madagascar, ukosefu wa usalama wa chakula uliongezeka baada ya kutokea tufani mbili, mwezi Januari na Februari zilizoharibu mazao ya biashara na kusababisha ugumu wa kufikisha misaada ya kibinadamu katika maeneo yaliyoathirika. Nchini Somalia, watu wanaokadiriwa kufikia milioni tano walikuwa na tatizo la chakula; ukame uliharibu vibaya sekta ya kilimo, ambayo inazalishahadi asilimia 90 ya bidhaa zinazouzwa nje ya nchi.

Migogoro ya kivita iliongeza ukubwa wa tatizo. Katika nchi ya Burkina Faso, makundi yenye silaha yalizingira miji na majiji takribani 46, na kuyazuia kupata bidhaa muhimu, kuzuia watu kwenda mashambani mwao na kuhujumu miundombinu ya maji. Mashirika ya kimataifa ya misaada yalisitisha msaada wa chakula kwa mkoa wa Tigray nchini Ethiopia kwa miezi sita kufuatia ushahidi kwamba misaada ilikuwa ikipelekwa kwingineko, yasemekana na mashirika ya serikali na jeshi. Zaidi ya watu milioni nne ambao tayari hawakuwa na usalama wa chakula waliathirika, na mamia inasemekana walikufa kwa matokeo yake.

Serikali zilichukua hatua kupambana na mfumuko wa bei na kuhakikisha chakula cha kutosha kinapatikana katika soko la ndani. Hatua hizo zilikuwa ni pamoja na Sierra Leone kutumia mpango wa kuongeza tija katika kilimo na kujitegemea kwa chakula, na Côte d'Ivoire kusitisha kwa muda uuzaji wa mchele na sukari nje ya nchi. Wakati huo huo, mwitikio wa kimataifa haukuwa wa kutosha. Msaada wa fedha za kigeni uliotolewa kwa ajili ya usalama wa chakula nchini Chad ulikuwa dola za Marekani milioni 96.9 hadi kufikia Septemba, ikiwa ni pungufu ya dola za Marekani milioni 128.1 kwa kiasi kilichokuwa kinahitajika. Nchini Sudan Kusini upungufu wa fedha kwa mradi wa misaada ya kibinadamu wa Umoja wa Mataifa ilimaanisha kuwa chakula

cha dharura kilitolewa kwa kupewa kipaumbele watu waliokuwa na upungufu mkubwa wa usalama wa chakula.

### HAKI YA ELIMU

Haki ya kupata elimu ilikosekana au kukumbwa na vikwazo vikali katika nchi zilizokuwa katika migogoro, hususan Burkina Faso, Cameroon, DRC na Niger. Nchini Burkina Faso, takribani shule 6,549 zilikuwa zimefungwa hadi kufikia mwezi Oktoba, huku takribani shule 539 tu zikifunguliwa katika mwaka husika, na kuathiri zaidi ya watoto milioni. Nchini Cameroon, takribani matukio 13 ya vurugu dhidi ya mashule yaliripotiwa katika mikoa ya kaskazini magharibi na kusini magharibi, ikiwemo kutekwa nyara watoto na walimu kati ya mwezi Januari na Julai, na takribani shule 2,245 zilifungwa. Nchini DRC, masomo ya watoto takribani 750,000 yalikatizwa katika majimbo mawili yaliyoathirika zaidi na machafuko mashariki mwa nchi hiyo. Maelfu ya shule yalishambuliwa na kulazimika kufungwa kutokana na hali mbaya ya usalama, au kutumika kama makazi kwa watu walioikimbia miji yao.

Aidha inatia moyo kwamba Mpango wa Elimu Bure wa Zambia kwa watoto wa umri wa kwenda shule za msingi ulianza mwezi Januari ambao chini yake walimu 4,500 zaidi walipewa ajira. Nchini Tanzania, kulikuwa na ongezeko la jumla la uandikishaji na viwango vya kujua kusoma na kuandika, na punguzo la vizuizi vya watoto kwenda shule. Hata hivyo, licha ya kufutwa kwa zuio la wasichana wanaopata mimba na akina mama vijana kuendelea na masomo katika shule za kawaida, ni wachache walioendelea na masomo.

### HAKI YA AFYA

Kupata matibabu katika nchi nyingi iliendelea kuwa changamoto. Huduma ya Afya ya Ghana ilieleza mwezi Februari kuwa wanawake wajawazito 27 katika manispaa ya Bawku walikufa kati ya mwaka 2021 na 2022 kutokana na kutoweza kupata huduma za matibabu. Nchini Afrika Kusini, mgomo wa mwezi Machi kuhusu mzozo wa mishahara, ulikwamisha upatikanaji wa huduma za matibabu na kusababisha vifo vinne, kulingana na Waziri wa Afya. Wakati huo huo, ugonjwa wa kuhara, kipindupindu, homa ya matumbo na milipuko ya magonjwa mengine iliripotiwa kutokea katika nchi za Congo, Sudan Kusini na kwingineko.

### KUHAMISHWA KWA NGUVU

Serikali ziliendelea kuhamisha watu kwa nguvu kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Nchini Benin, maelefu ya watu waliokuwa wamehamishwa kwa nguvu kuhusiana na miradi ya utalii katika mwambao, kati ya miji ya Cotonou na Ouidah, walilalamika kuhusu kutopewa fidia ya kutosha. Katika jimbo la Lualaba nchini DRC, upanuaji wa migodi ya kobalti na shaba, ukichochewa na ongezeko la hitaji la soko la dunia kwa ajili ya madini ya kusafirisha nishati, ulichochea kuhamishwa kwa nguvu kwa maelfu ya watu kutoka katika miji na mashamba yao.

Katika jimbo la Hoima nchini Uganda, vikosi vya usalama vilitumia vurugu katika zoezi la kuhamisha kwa nguvu familia zipatazo 500 kutoka ardhi yao kupisha ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP). Nchini Tanzania, wakazi wa asili 67 wa jamii ya Wamaasai walitiwa mbaroni, hususan katika kijiji cha Endulen, kwa kukataa kuondoka katika ardhi ya mababu zao chini ya mipango inayoendelea ya kuwahamisha kwa nguvu kwa ajili ya uanzishaji wa pori tengefu katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

**Serikali lazima zichukue hatua mara moja kushughulikia matatizo ya kiuchumi na kijamii, ili kuhakikisha kwamba rasilimali zinakuwepo, kulingana na wajibu wake mkuu wa kimsingi, kuwapatia watu wao haki zao za kiuchumi na kijamii.**

## HAKI ZA WATU WALIOPOTEZA MAKAZI NCHINI MWAO, WAKIMBIZI NA WAHAMAJI

Takribani watu milioni saba walikadiriwa kuwa wamepoteza makazi yao nchini DRC, ambayo ni idadi kubwa kabisa barani Afrika. Nchi hiyo ilitoa hifadhi kwa wakimbizi 500,000 kutoka maeneo yenye mapigano ya kivita na mauaji katika nchi nyingine za Afrika. Kati ya mwezi Januari na

Agosti, watu takribani 45,000 walikimbia kutoka DRC kwenda nchi za jirani, ikiwemo Uganda ambayo inatoa hifadhi kwa wakimbizi milioni 1.6, ambayo ni idadi kubwa zaidi ya wakimbizi barani Afrika.

Zaidi ya watu milioni 5.8 walipoteza makazi yao nchini Sudan kuanzia mwezi Aprili, na kuifanya nchi hiyo kuwa eneo la mgogoro mkubwa wa watu waliopoteza makazi yao duniani kwa mwaka 2023. Zaidi ya watu milioni 4.5 walipoteza makazi yao kati ya mwezi Aprili – mapigano yalipoanza – na Oktoba, wakati raia takribani milioni 1.4 wa Sudan na mataifa mengine walikimbilia katika nchi nyingine. Hata hivyo, baadhi ya nchi zilikataa kuwapokea raia wa Sudan waliokuwa wakitafuta hifadhi ya wakimbizi; serikali ya Misri iliwataka raia wote wa Sudan kupata visa iliyotolewa na ubalozi mdogo wa Misri nchini Sudan, na kuweka kigezo cha ziada cha kupata idhini ya kiusalama kwa wavulana na wanaume wote wa kati ya miaka 16 hadi 50.

Nchini Niger, wakimbizi na wahamiaji takribani 9,000 waliokuwa wamerudishwa makwao na serikali ya Algeria waliwasili kijiji cha mpakani cha Assamaka kati ya mwezi Januari na Aprili. Nchini Malawi, polisi waliwakamata mamia ya wakimbizi kutoka nyumba na biashara zao katika mji mkuu, na kuwapeleka katika kambi ya wakimbizi ya Dzaleka.

**Serikali lazima ziheshimu wajibu wao wa kutoa hifadhi kwa wakimbizi, watu wanaotafuta hifadhi na wahamaji, ikiwemo kuheshimu haki ya kupata hifadhi ya wakimbizi na kutowarejesha watu walikokimbia.**

## UBAGUZI

### HAKI ZA WANAWAKE NA WASICHANA

Madhara hatari ya ukeketaji wa wanawake yalidhihirika pale msichana wa miaka miwili alipokufa baada ya kukeketwa nchini Sierra Leone. Ndoa za utotoni, za mapema na za kulazimishwa ziliendelea kuwepo katika kanda. Takribani asilimia 29 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 20 na 24 nchini Zambia walikuwa wameshaolewa kabla ya kufikisha miaka 18. Tukio la binti wa miaka 16, Nazira aliyeamua kukatisha maisha yake kuepuka ndoa ya lazima liliangazia madhara ya ndoa za mapema nchini Niger.

Kulikuwa na maendeleo chanya kadhaa ya kutunga sheria. Nchi ya DRC ilitunga sheria iliyofanya suala la unyanyasaji kijinsia na unyanyapaa kuwa kosa la jinai. Nchini Sierra Leone, sheria mpya ilitaka asilimia 30 ya nafasi za utumishi wa umma kushikwa na wanawake. Nchini Afrika Kusini, mswada unaopendekeza kuundwa chombo cha kusimamia mpango mkakati kuhusu ukatili wa kijinsia, uliwasilishwa kwa ajili ya watu kutoa maoni yao.

### HAKI ZA WASAGAJI, MASHOGA, WATU WANAOUVUTIWA KIMAPENZI NA WATU WA JINSIA ZOTE MBILI, WATU WENYE JINSIA TOFAUTI NA JINSIA YAO YA ASILI, WATU WENYE JINSIA MBILI (LGBTI)

Baadhi ya nchi zilichukua hatua kutunga sheria dhidi ya mapenzi ya jinsia moja. Nchini Uganda sheria mpya ambayo inatoa adhabu ya kifo kwa kosa la kufanya mapenzi ya jinsia moja, ilifuatiwa na taarifa za ongezeko la kushambuliwa kwa watu wa LGBTI. Nchini Kenya, Mbunge mmoja alipendekeza kutungwa sheria ambayo itafanya kuwa kosa la jinai kwa watu wa jinsia moja kufanya mapenzi kwa ridhaa yao. Nchini Ghana, bunge lilipitisha mswada wa kupinga mapenzi ya jinsia moja. Nchini Eswatini, serikali ilidharau amri ya mahakama ilipokataa kusajili chama cha LGBTI.

Kutiwa mbaroni na kuwekwa kizuizini wapenzi wa jinsia moja lilikuwa jambo la kawaida. Nchini Burundi, watu 24 walitiwa mbaroni mwezi Februari huko Gitega kwenye kongamano la ujumuishwaji kiuchumi. Wao, na watu wengine wawili ambao baadaye waliongezwa kwenye kesi walishtakiwa kwa kosa la "ushoga" na "kuhamasisha ufanyaji ngono uliopitiliza." Saba kati yao walitiwa hatiani mwezi Agosti na tisa kati yao ambao hawakukutwa na hatia, hawakuachiwa huru mara moja, na mmoja wao alifia chini ya ulinzi wa polisi. Nchini Nigeria, wanaume 69 walifikishwa mahakamani kwa kosa la jinai la kuandaa ndoa ya wapenzi wa jinsia moja katika jimbo la Delta wakati kundi lingine la wanaume 59 na wanawake 17 walitiwa nguvuni katika jimbo la Gombe kwa madai ya kuandaa sherehe ya siku ya kuzaliwa iliyohusisha "mashoga."

Pia kauli za kupinga mapenzi ya jinsia moja ziliongezeka katika nchi za Botswana, Cameroon, Ethiopia, Kenya, Malawi na Tanzania. Katika nchi za Botswana na Malawi, mamia ya waandamanaji, wakiwa wanaungwa mkono na makundi ya kidini na maafisa wa serikali, waliandamana dhidi ya suala la kufanya mapenzi ya jinsia moja kwa watu wazima wanaoamua kufanya hivyo kwa hiari yao kutokuwa kosa la jinai. Nchini Cameroon serikali ilitishia kusimamisha usajili wa vyombo vya habari endapo vitarusha hewani vipindi "vinavyochochea ushoga." Nchini Ethiopia, kampeni dhidi ya watu wa LGBTI kwenye mtandao na nje ya mtandao ilizinduliwa ikiongozwa na watu mashuhuri, viongozi wa dini na wasanii maarufu. Nchini Tanzania, Waziri wa Elimu alipinga marufuku vitabu vyenye maadhui ya LGBTI kutumika mashuleni.

Aidha inatia moyo kwamba mahakama kuu ya Namibia iliamua kuwa wenza ambao ni raia wa Namibia wangeweza kuhalalisha hadhi yao ya uhamiaji kulingana na ndoa za jinsia moja zilizofungwa nje ya nchi; na mahakama kuu ya Kenya ilithibitisha haki ya watu wa LGBTI ya uhuru wa kujumuika.

### WATU WENYE UALBINO

Uhalifu dhidi ya watu wenye ualbino, ikiwemo majaribio ya kuwateka nyara, mashambulio ya kimwili na ufukuaji wa makaburi yao, uliongezeka Malawi. Nchini Angola, Mpango Kazi wa Kitaifa kwa ajili ya Kulinda na Kuendeleza Haki za Binadamu za Watu wenye Ualbino ulianza kutumika rasmi.

**Serikali lazima zidhibiti haraka aina zote za ubaguzi wa kijinsia na ukatili dhidi ya wanawake na wasichana, ikiwemo kuchunguza kiini cha tatizo, na kuongeza juhudi za kukomesha tabia zenye madhara. Serikali lazima ziimarishe ulinzi wa haki za watu wa LGBTI ikiwemo kutunga sheria, na kuchunguza kikamilifu taarifa za kutotenda haki na kuwafikisha watuhumiwa mbele ya sheria.**

## HAKI YA KUWA NA MAZINGIRA SALAMA

Nchi kadhaa ziliathirika kutokana na matukio ya hali mbaya ya hewa, ambayo ukubwa na kasi ya utokeaji wake inaweza kuhusishwa na mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, serikali hazikuwa zimejiandaa sawa sawa kukabiliana na kutokea taratibu au haraka kwa matukio ya hali ya hewa kwenye kanda yote. Katika miezi ya Februari na Machi, Kimbunga Freddy kiliathiri mamilioni ya watu katika nchi za Malawi na Msumbiji, kikiua watu 679 na 453, kwa mfuatano huo. Mafuriko yaliua watu wengi katika nchi nyingine kadhaa, zikiwemo DRC na Rwanda. Mwezi Septemba, Mkutano wa kwanza wa Kilele kuhusu Tabianchi Afrika ulifanyika Nairobi kuweka msimamo wa pamoja wa Afrika kabla ya majadiliano kwenye Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Tabianchi (COP28).

**Serikali lazima zichukue hatua za haraka kutoa ulinzi dhidi ya hatari na madhara ya tatizo la mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha utayari wao kukabiliana na hali mbaya ya hewa, ikiwemo kutafuta msaada wa kimataifa na fedha za tabianchi kutoka nchi zilizoendelea kwa ajili ya kutumia sera za kukinga na kuenenda na hali, na kufidia hasara na uharibifu waliosababishiwa watu maskini zaidi.**

## HAKI YA KUPATA UKWELI, HAKI NA FIDIA

Kufuatia kampeni ya kejeli ya serikali ya Ethiopia kuzuia mipango ya upatikanaji haki na uwajibikaji, Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ilisitisha mapema zaidi mamlaka ya Tume yake ya Uchunguzi wa hali ya mkoa wa Tigray, bila ya kuchapisha taarifa yoyote. Serikali pia ililenga Tume ya Kimataifa ya Umoja wa Mataifa ya Wataalam wa Haki za Binadamu ya Ethiopia (ICHREE), jambo lililosababisha nchi wanachama kwenye Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kutoa azimio la kuendeleza mamlaka ya ICHREE. Burundi ilisusia kikao cha kujadili hali yake kwenye Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa ikipinga kuwepo kwa mtetezi wa haki za binadamu aliyekuwa amehukumiwa bila ya kuwepo mahakamani kwa mashtaka ya uongo ya kushiriki katika jaribio la mapinduzi la mwaka 2015 huku Tanzania ikizuia

ujumbe wa UNESCO wa kutafuta ukweli kutembelea Ngorongoro kuchunguza taarifa za kuhamisha watu kwa nguvu na ghasia dhidi ya Watu wa Asili wa jamii ya Wamaasai.

Nchi kadhaa zilianzisha au zilifikiria kuanzisha michakato ya ukweli na maridhiano, aghalabu kwa gharama ya kutafuta haki na uwajibikaji kwa wahanga wa uhalifu chini ya sheria za kimataifa na ukiukwaji na uvunjaji mwingine mkubwa wa haki za binadamu. Serikali ya DRC ilianza kutumia Mswada wa Sera ya Kitaifa ya Mpito ya kutafuta Haki, na serikali ya Ethiopia ilianza majadiliano ya kutumia sera kama hiyo.

Nchini Sudan Kusini, Baraza la Mawaziri lilipitisha miswada miwili ya kuunda Tume ya Ukweli, Maridhiano na Uponaji na Mamlaka ya kulipa Fidia, ambayo ilikuwa bado haijapelekwa bungeni kwa majadiliano. Hata hivyo liliendelea kuzuia uundwaji wa Mahakama yenye Mamlaka ya Kitaifa na Kimataifa huko Sudan Kusini. Serikali ya Gambia ilikubali kuunda Mahakama yenye Mamlaka ya Kitaifa na Kimataifa kuendesha kesi za waliohusika katika uvunjaji mkubwa wa haki za binadamu wakati wa utawala wa Rais Yahya Jammeh.

Watuhumiwa kadhaa wa uhalifu chini ya sheria ya kimataifa walikamatwa. Mahakama Maalum ya Jinai ya nchi ya CAR ilitangaza kukamatwa kwa watu wanne wanaoshtakiwa kwa uhalifu wa kivita na/au uhalifu dhidi ya binadamu. Hatua zilichukuliwa kuwafikisha mbele ya sheria watuhumiwa wawili wa mauaji ya kimbari: Fulgence Kayishema alikamatwa upya kwa hati mpya ya kumkamata ambayo itawezesha kumhamishia kwenye Mahakama ya Umoja wa Mataifa ya kushughulikia Umaliziaji wa Kesi za baadhi ya Mauaji ya Kimbari ya Rwanda na Yugoslavia iliyoko Tanzania (*International Residual Mechanism for Criminal Tribunals -IRMCT*) wakati Théoneste Niyongira alipelekwa Rwanda kutoka Malawi.

**Serikali lazima ziimarishe juhudi za kupambana na suala la uvunjaji wa sheria bila kuogopa kuadhibiwa kwa kufanya uchunguzi wa haraka, wa kina, wa kujitegemea, usio na upendeleo, wenye kuzaa matunda na wa wazi kuhusu uhalifu chini ya sheria ya kimataifa na uvunjaji na ukiukwaji mwingine mkubwa wa haki za binadamu, kuwafikisha watuhumiwa mbele ya sheria na kuhakikisha wahanga wanapata fidia stahiki.**

# KENYA

**Jamhuri ya Kenya**

**Maafisa wa polisi waliendelea kutojali sheria kwa kufanya mauaji ya makusudi na kupotezwa kwa nguvu bila kujali sheria. Haki ya kukusanyika kwa amani ilikiukwa, na takribani waandamanaji 57 waliuawa na mamlaka katika jaribio la kuzima upinzani. Serikali ilishindwa kuchukua hatua kulinda haki ya kuishi. Mashtaka dhidi ya maafisa wa polisi wanaoshtakiwa kufanya uhalifu wa mauaji yalihairishwa mara kwa mara. Haki za wapenzi wa jinsia moja (LGBTI) zilihatarishwa baada ya mapendekezo ya sheria ya chuki dhidi yao. Mabadiliko makubwa ya kodi na kuongezeka kwa gharama za maisha vilitishia uwezo wa Wakenya kumudu maisha yao. Pendekezo la kuongeza ada ya bima binafsi ya maisha lilitishia haki ya kupata matibabu kwa wale ambao wasingeweza kumudu gharama. Watu milioni tano walikuwa katika hatari ya kukabiliwa na upungufu mkubwa wa usalama wa chakula kutokana na ukame. Serikali ilishindwa kulinda haki ya faragha kwa maelfu ya Wakenya ambao bila kujua waliuza taarifa zao binafsi kwa kampuni ya Worldcoin. Bunge lilichukua hatua za kukomesha hukumu ya kifo.**

### UTANGULIZI

Mwaka wa kwanza wa Rais Ruto madarakani ulidhihirishwa na kuongezeka kwa gharama za maisha na kusababisha maandamano nchi nzima.

Mnamo Oktoba 9, mahakama kuu iliweka zuio la muda kupeleka maafisa wa polisi 1,000 kusaidia Jeshi la Polisi la taifa la Haiti kupambana na magenge ya uhalifu yaliyoshamiri nchini humo, ili kusubiria matokeo ya ombi lililowasilishwa mahakamani hapo na Chama cha *Thirdway Alliance*. Mashirika ya kijamii pia yalipinga kupelekwa kwa askari hao, yakitoa sababu za Maafisa wa Polisi wa Kenya kuendelea kutumia nguvu kinyume cha sheria, hasa dhidi ya waandamanaji. Siku chache baadaye baraza la mawaziri lilipitisha azimio kupeleka maafisa hao Haiti, lakini mnamo Oktoba 24, mahakama kuu ikaongeza muda wa zuio lake. Upelekaji wa polisi hao unaungwa mkono na Umoja wa Mataifa na serikali ya Marekani, na uliidhinishwa na bunge mwezi Novemba lakini haujatekelezwa hadi kufikia mwishoni mwa mwaka.

## MAUAJI YA MAKUSUDI NJE YA UTARATIBU WA SHERIA NA KUPOTEZWA KWA NGUVU

Kulikuwa na mauaji 136 ya makusudi bila ya kufuata sheria katika mwaka huo. Wengi wa wahanga walikufa wakiwa mikononi mwa polisi au walikuwa wameonekana mara ya mwisho wakiwa mikononi mwa polisi. Ni kesi 28 tu, zikiwemo za mwaka uliopita ndizo zilipelekwa mahakamani.

Kulikuwa na maendeleo kidogo sana ya kuwawajibisha polisi kwa mauaji ya makusudi bila ya kufuata sheria, ikiwemo kesi ya miili ipatayo 37 iliyopatikana Mto Yala, na kwingineko mwaka 2022. Serikali ilishindwa kutekeleza Sheria ya Taifa ya Huduma ya Mchunguzi wa Maiti, ambayo ina kipengele cha kuanzisha ofisi ya mchunguza maiti mkuu ili kuratibu uchunguzi wa vifo visivyo na maelezo.

Mwezi Februari, Lilian Waithera aliuawa na mshambuliaji asiyefahamika wakati akisaidia katika kesi ya kupambana na ufisadi dhidi ya maafisa waandamizi wa serikali. Mtuhumiwa alikamatwa lakini hakukuwa na maelezo zaidi kutoka serikalini kuhusu upelelezi wa kifo chake.

Watu kumi walipotezwa kwa nguvu. Serikali ilishindwa kufanya upelelezi wa haraka, wa kina, usio na upendeleo, wa kujitegemea, wa wazi na wenye matokeo stahiki kwa kupotezwa kwa nguvu, au mauaji ya makusudi bila ya kufuata sheria, au kuridhia Mkataba wa Kimataifa dhidi ya kupotezwa kwa nguvu.

## UHURU WA KUJIELEZA NA KUKUSANYIKA

Kati ya mwezi Machi na Julai, polisi walitumia nguvu kupita kiasi kutawanya waandamanaji na kuzuia maandamano dhidi ya kuongezeka kwa gharama za maisha na madai ya kasoro katika uchaguzi wa 2022. Kulingana na Mamlaka Huru ya Usimamizi wa Polisi, watu 57 waliuawa katika maandamano hayo. Amnesty International ilithibitisha vifo 30 kati ya hivyo, ikivihusisha na kupigwa risasi za moto, majeraha yaliyosababishwa na vifaa butu, na kuvuta moshi utokanao na mabomu ya machozi. Maafisa wa polisi pia walitumia maji ya kuwasha kushambulia waandamanaji. Wakati wa kipindi hicho, watoa huduma ya kwanza katika hali ya dharura, waandishi wa habari na watetezi wa haki za binadamu hawakuweza kuingia katika maeneo yao ya kazi kutokana na barabara kufungwa na vurugu katika njia zao za kawaida. Kwa hiyo, wafanyakazi wa afya hawakuweza kutoa huduma ya dharura.

Huduma ya Kitaifa ya Polisi ilikataa kukubali maombi kadhaa ya kufanya maandamano, na kutamka kwamba maandamano yaliyopangwa ni kinyume cha sheria. Serikali ilijaribu zaidi kuzuia haki ya kukusanyika kwa amani kwa kuongeza vifungu katika Sheria ya Amani ya Umma, ambavyo vilipingana na kinga ya kikatiba.

Mwezi Oktoba, polisi walitawanya angalau mkutano mmoja binafsi ulioandaliwa kupinga vita vya Israel vinavyoendelea huko Gaza. Serikali ilithibitisha kuiunga mkono Israel.

## HAKI YA KUISHI

Kwa miaka sita, serikali ilishindwa kuchunguza ukatili dhidi ya mamia ya watu, ambao inadaiwa ulifanywa na kanisa la Good News International Ministries (GNIM) katika Kaunti ya Kilifi. Mwezi Machi, yaligundulika makaburi ya halaiki yakiwa na takribani watu 428, wakiwemo takribani watoto tisa, kulingana na ripoti ya kamati ya seneti. Vyanzo vya vyombo vya habari vilihusisha vifo hivyo na viongozi wa GNIM. Uchunguzi wa maiti ulibainisha kuwa walikuwa wamekosa chakula, wamepigwa na silaha butu na kunyongwa. Mwezi Aprili, baadhi ya watuhumiwa walikamatwa na wanakabiliwa na mashtaka yanayohusiana na ugaidi. Miongoni mwao ni kiongozi wa kanisa hilo aliyehukumiwa kifungo cha miezi 12 jela kwa kuendesha studio ya filamu na kutoa filamu bila leseni.

## HAKI YA KUPATA UKWELI, HAKI NA FIDIA

Kumekua na hatua chache sana mahakamani kuhusu mashtaka dhidi ya maafisa wa polisi wanaoshtakiwa kwa kuua kinyume cha sheria. Kesi ya afisa wa polisi anayeshtakiwa kwa kuua wavulana wawili ambao hawakuwa na silaha huko Eastleigh, Nairobi, mwaka 2017 bado haijaanza kusikilizwa. Kesi ya afisa wa polisi anayeshtakiwa kwa kumuua Yassin Moyo, mvulana wa miaka 14 mwaka 2020 wakati wa amri ya kukaa ndani kipindi cha Uviko-19, bado haijaanza kusikilizwa, ikiwa imeahirishwa mara kadhaa. Kesi dhidi ya afisa ambaye anashtakiwa kwa kumuua Carilton Maina mwaka 2018 katika eneo la Kibera Laini Saba iliahirishwa zaidi ya mara 10. Evans Njoroge, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Meru, alipigwa risasi kwa karibu wakati wa maandamano ya amani mwaka 2018. Kesi dhidi ya afisa wa polisi anayeshtakiwa kwa kumfuatilia na kumpiga risasi bado haijakamilika.

Kamati ya Kitaifa ya Mazungumzo (NDC), iliyoundwa kukusanya maoni ya Wakenya, na kuishauri serikali kuhusu masuala ya kitaifa, ikiwemo maandamo ya “kupinga serikali” (angalia hapo juu, Uhuru wa kujieleza na kukusanyika), ilishindwa kushughulikia kikamilifu ukatili wa polisi na fidia kwa watu 57 waliouawa na wengine wengi waliojeruhiwa katika maandamano.

## HAKI ZA WAPENZI WA JINSIA MOJA (LGBTI)

Mnamo Februari, Mahakama ya Upeo ilithibitisha haki ya uhuru wa kujumuika kwa watu wanaofanya mapenzi ya jinsia moja, na kuilekeza Bodi ya Kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kusajili vyama vya LGBTI bila ubaguzi. Hukumu hiyo iliamsha hasira, ikiwemo vitisho vya kifo

dhidi ya wapenzi wa jinsia moja. Mwezi Aprili, Mbunge wa Mji wa Homa Bay, alipendekeza bungeni Mswada wa Sheria ya Kulinda Familia, ambayo kama ikipitishwa, itafanya kuwa kosa la jinai kwa wapenzi wa jinsia moja kufanya ngono kwa ridhaa yao na kutoa adhabu ya kifo kwa "ushoga uliokithiri."

Mwezi Januari, Edwin Chiloba, aliuawa katika kile kinachodaiwa na Serikali kuwa ni kutokana na ukatili wa kimapenzi wa mwenza wake. Idara za serikali zilishindwa kuchunguza madai kwamba kuuawa kwake kulichochewa na hulka yake kingono.

## HAKI ZA KIUCHUMI NA KIJAMII

Serikali haikutimiza ahadi yake ya kuweka viwango vya kodi vya juu zaidi kwa matajiri. Mwezi Juni, bunge lilipitisha bajeti, ambayo ilianzisha kodi mpya na kupandisha gharama ya bima ya afya na michango ya malipo ya uzeeni kwa wafanyakazi wanaolipwa mishahara. Pia ilianzisha ushuru wa nyumba na kodi ya ongezeko la thamani kwa baadhi ya bidhaa, na hivyo kupandisha mara mbili bei ya mafuta na bidhaa muhimu.

Baadaye mwezi Juni, Bajeti hiyo ilipingwa kwenye mahakama kuu, katika kitengo cha Katiba na Haki za Binadamu ambayo iliamuru Hazina ya Taifa kutotekeleza nyongeza hizo mpya. Hata hivyo, Waziri wa Hazina ya Taifa na Mipango ya Uchumi alikata rufani dhidi ya hukumu hiyo kwa misingi kwamba ingesababisha hasara ya shilingi nusu bilioni za Kenya (takribani dola za Marekani milioni 3.25) kwa siku. Mwezi Julai, mahakama ya rufani ilitengua amri ya mahakama kuu, na hivyo kufungua njia kwa kodi mpya kuanza kutumika.

## HAKI YA AFYA

Serikali ilipendekeza ongezeko la asilimia 2.75 katika michango ya bima ya afya kwa wafanyakazi wote wanaolipwa mshahara. Kuna uwezekano ongezeko hilo litaathiri uwezo wa kiuchumi wa Wakenya wengi.

Mnamo Oktoba 20, serikali ilizindua mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kuhakikisha watu wote wanapata matibabu, kuendana na ilani yao ya mwaka 2022.

Ripoti ya Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi ya mwaka 2023 ilielezea matukio ya rushwa katika utaratibu wa kutoa huduma ya afya.

## HAKI YA KUWA NA MAZINGIRA SALAMA

Mwezi Julai, serikali iliondoa katazo la kukata miti ya kibiashara lililodumu kwa miaka mitano, ikiwa ni tishio kwa miti na misitu asilia.

Mwezi Septemba, Kenya ilikuwa mwenyeji wa Wiki ya Tabianchi na Mkutano wa Kilele Barani Afrika wa mwaka wa 2023, ulioweka Azimio la Nairobi ambalo lilitoa wito wa kutumia makadirio ya kifedha kugharamia miradi mahsusi kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, lakini ambalo kwa namna nyingi lilishindwa kutoa kipaumbele kwa haki za binadamu na usawa wa ugharamiaji wa mzigo wa mabadiliko ya tabianchi kwa nchi za Afrika.

Ukame kaskazini mwa Kenya uliendelea kwa mwaka wa nne, na kuwaweka watu milioni tano wakiwemo wakimbizi katika hatari ya ukosefu mkubwa wa usalama wa chakula.

Wakimbizi katika kambi za wakimbizi za Dadaab na Kakuma waliendelea kuwa katika hatari ya kuathirika na matukio mabaya ya hali ya hewa. Kambi hizo zipo katika eneo la ukame na ukame kiasi, na kufanya watu waishi katika eneo lenye joto kali na mvua kidogo kwenye eneo dogo na lenye msongamano mkubwa wa watu. Upatikanaji wa huduma ya vyoo, maji, chakula na mahitaji mengine muhimu kwa wakimbizi ni mdogo sana.

## HAKI YA KUWA NA FARAGHA

Kufikia mwezi Juni, serikali ya Kenya ilikuwa imeweka kidijitali huduma 5,000 za serikali, jambo ambalo lilizua wasiwasi miongoni mwa Wakenya kuhusu haki za faragha. Mwezi Julai tovuti ya serikali ilipata shambulio la kidijitali na kushindwa kutoa huduma (shambulio ambalo dhumuni lake ni kufanya kompyuta au mtandao ushindwe kufanya kazi), jambo lililozua mashaka zaidi kuhusu uwezo wa serikali kuhakikisha uwepo wa faragha.

Mwezi Septemba, zaidi ya Wakenya 350,000 "waliuza" taarifa za mboni za macho yao (iris scans) kwa WorldCoin, kampuni ya Marekani, kwa kubadilishana na sarafu ya kidijitali yenye thamani ya shilingi 7,000 za Kenya (takribani dola 45 za Marekani). Mwezi Oktoba, amri ya mahakama ilisitisha utaratibu huo, na Ofisi ya Kamishna wa Kulinda Data ilifuta usajili wa WorldCoin, ikinukuu kuvunjwa kwa sheria ya kulinda data ya mwaka 2019 (Data Protection Act 2019).

## ADHABU YA KIFO

Mahakama za Kenya ziliendelea kutoa adhabu ya kifo. Mwezi Septemba, Mbunge alipeleka miswada ya kufuta hukumu ya kifo kwenye sheria. Kifungu cha 26(3) cha katiba ambacho ndicho kinaruhusu adhabu ya kifo, na Sheria ya Majeshi ya Ulinzi havikuhusishwa katika marekebisho hayo. Hata hivyo, Kamati ya Bunge ya Haki na Masuala ya Sheria ilianzisha mchakato wa kufanya mapitio ya sheria kuhakikisha kwamba sheria zote zinazotoa adhabu ya kifo zinafanyiwa marekebisho ya kisheria.

# TANZANIA

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Serikali ilikandamiza upinzani wa amani, ikiwatia mbaroni kiholela wakosoaji wa mpango wa Rais wa maendeleo, wanachama wa upinzani na wale wanaohusiana na upinzani, wanasheria, Watu wa Asili wa jamii ya Wamaasai na wanaharakati. Bunge liliifanyia marekebisho Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari. Mahakama Kuu iliwapa ushindi Wamaasai wa Loliondo kuhusiana na kuhamishwa kwa nguvu kutoka katika ardhi ya mababu zao. Kampuni ya East African Crude Oil Pipeline (EACOP) Ltd ilipewa leseni kujenga bomba lenye urefu wa kilomita 1,443. Serikali ilikataa kuuruhusu ujumbe wa kimataifa wa kutafuta ukweli kufanya tathmini ya ukiukwaji wa haki za binadamu dhidi ya Wamaasai wa Ngorongoro. Uamuzi wa kuondoa tamko la mahakama ambalo lingewezesha watu binafsi na asasi za kiraia kwenda Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu bado unaendelea. Licha ya kuwepo maboresho katika upatikanaji wa elimu, bado kulikuwa na idadi ndogo ya wasichana wanaoendelea na masomo kutokana na umaskini, mimba za utotoni na ukatili wa kijinsia mashuleni. Matumizi ya lugha ya chuki dhidi ya wapenzi wa jinsia moja (LGBTI) yaliongezeka.**

### UTANGULIZI

Oktoba 2022, Rais alisaini mkataba wa makubaliano ya serikali na ufalme wa Dubai wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) wa kushirikiana kuendeleza, kusimamia na kuendesha bandari za Tanzania na miundombinu mingine inayohusiana nazo. Mnamo Juni 10 bunge liliidhinisha mkataba huo.

Mwezi Februari serikali ilizindua utaratibu wa kupata maoni ya wananchi kuhusu marekebisho ya katiba na sheria nyinginezo.

## UHURU WA KUJIELEZA, KUJUMUIKA NA KUKUSANYIKA

Mwezi Januari, Rais aliondoa katazo la jumla lenye vipengele vya adhabu, lililowekwa mwaka 2016 na Rais aliyefia madarakani la kukataza vyama vya siasa kufanya mikutano na shughuli nyingine za siasa. Wanasiasa mashuhuri ambao huko nyuma walikuwa wamepuuzia katazo hilo, walikuwa wamekamatwa bila kuzingatia sheria na kuwekwa kizuizini. Hata hivyo, serikali iliendelea kukandamiza shughuli za kisiasa, wakosoaji wa miradi ya serikali na wale waliopinga kuhamishwa kwa nguvu, ikiwemo kutiwa mbaroni bila kuzingatia sheria, kuwekwa kizuizini na kunyanyaswa.

Takribani watu 12 walikamatwa kati ya mwezi Juni na Desemba kwa kukosoa mkataba wa Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu. Waliokamatwa waliachiwa bila masharti yoyote baada ya kushikiliwa kwa siku chache. Rugemeleza Nshala, mwanaharakati na rais wa zamani wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika, ambaye pia alikuwa ameukosoa mkataba huo, alikimbia nchini mwezi Julai baada ya kupewa vitisho na polisi na vitishio vya kifo kwenye simu yake kutoka vyanzo visivyojulikana.

Mwezi Juni, bunge lilipitisha mabadiliko chanya kwenye Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari, ikiwemo kufuta kipengele cha kazi ya uandishi wa habari kuwa kosa la jinai katika utendaji kazi wake, kupunguza adhabu na faini kwa wanaotiwa hatiani kwa makosa ya kashfa na kuziondolea mahakama uwezo wa kuamuru kukamatwa kwa vifaa vya vyombo vya habari.

Mnamo Julai 14, wakili wa kujitegemea na mwanaharakati Boniface Mwabukusi, na mwanaharakati wa kisiasa Mdude Nyagali walikamatwa ikiwa zimepita siku kadhaa tangu walipofanya mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam ambapo walikosoa mkataba kati ya Tanzania na UAE. Mnamo Agosti 12, walikamatwa tena wakati wakiwa njiani kuelekea Dar es Salaam na kupelekwa Kituo cha Kati cha Polisi jijini Mbeya. Siku iliyofuata, polisi walimkamata Willibrod Slaa, mbunge wa zamani na mwanadiplomasia, nyumbani kwake jijini Dar es Salaam na kumpeleka Kituo cha Polisi cha Mbweni. Watatu hao, ambao waliachiwa Agosti 18 chini ya masharti magumu ya kuripoti polisi, walikuwa wakikabiliwa na mashtaka ya uhaini.

Mnamo Septemba 6, mkuu wa polisi wa wilaya ya Ngorongoro, mkoani Arusha alitoa onyo dhidi ya chama kikuu cha upinzani cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kutofanya mikutano ya hadhara iliyokuwa imepangwa kufanyika Septemba 8 na 9 katika tarafa ya Loliondo. Serikali ilitoa sababu za kiusalama kuhalalisha katazo hilo lakini haikutoa sababu zaidi; ilidai katazo hilo lilikuwa ni kulingana na kanuni za Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCA).

Mnamo Septemba 10, polisi walimkamata kiongozi wa upinzani Tundu Lissu kwa kufanya "mkusanyiko usio halali" baada ya kushiriki mkutano wa kisiasa katika tarafa ya Loliondo. Alikamatwa alipokuwa akijaribu kuingia eneo la NCA kuzungumza na Wamaasai waliokuwa wakishiriki katika mkutano mwingine. Aliachiwa siku hiyo hiyo bila kufunguliwa mashtaka.

## KUHAMISHWA KWA NGUVU

Takribani Wamaasai 67 walikamatwa katika mwaka huo, wengi wao wakiwa wakazi wa kijiji cha Endulen, tarafa ya Ngorongoro, kwa kukataa kuondoka katika ardhi ya mababu zao chini ya mpango wa kuhamisha watu kwa nguvu ili kuanzisha pori tengefu ndani ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Baadhi walishikiliwa kwa saa chache na wengine kwa siku kadhaa.

Mnamo Agosti 7, mahakama kuu jijini Mbeya ilitoa hukumu ya kutupilia mbali agizo la serikali kuwaondoa takribani watu 21,000 kutoka kwenye ardhi yao katika vijiji vitano kati ya 39 vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha katika wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya. Serikali ilisema ilikuwa ikihitaji ardhi hiyo kwa ajili ya eneo la hifadhi ya wanyamapori ndani ya hifadhi ya taifa. Kesi hiyo mbele ya mahakama kuu ilifunguliwa mwezi Januari na wakulima wadogo 852 kutoka Marili, baada ya kupewa notisi ya kuhamishwa mnamo Oktoba 2022 iliyotolewa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambayo ilisema vijiji hivyo vipo ndani ya hifadhi ya taifa. Muda mfupi kabla ya hukumu ya mahakama kuu, Kamishna Msaidizi wa Ardhi wa Kanda ya Mbeya alikuwa ameiambia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwamba serikali, kimsingi, ilikuwa imerejesha kilomita za mraba 744.32 za ardhi hiyo kwa jamii katika wilaya ya Mbarali.

Mnamo Septemba 19, mahakama kuu ya mkoa wa Arusha ilifikia uamuzi kuwa Pori Tengefu la Pololeti lililopo tarafa ya Loliondo lilianzishwa kinyume cha sheria. Juni 17, 2022, Waziri wa Maliasili na Utalii alikuwa ametangaza Pololeti kuwa "pori tengefu" – eneo lilotengwa maalum kwa ajili ya kuhifadhi wanyamapori – kuhalalisha zoezi la kuwahamisha kwa nguvu Wamaasai kutoka kilomita za mraba 1,500 za ardhi yao. Jamii hiyo ilipinga uamuzi huo katika mapitio ya kesi iliyofunguliwa mnamo Novemba 2022. Mahakama kuu iliamua ya kwamba serikali haikuwashirikisha wakazi ilipotoa tamko lake, na hivyo kufanya mchakato wote kuwa batili.

Hadi mwishoni mwa mwaka, familia za Kimaasai zipatazo 100 ziliendelea kuishi katika hali duni kwa kutegemea tu kujikimu kimaisha kutoka vijiji vya Oloolaimutia na Olpusimoru katika kaunti ya Narok, Kenya. Walikimbilia huko na mifugo yao baada ya maboma yao kuharibiwa wakati wa zoezi la kuwahamisha kwa nguvu mnamo Juni 2022 katika tarafa ya Loliondo.

## HAKI YA KUWA NA MAZINGIRA SALAMA

Shirika la Fedha Duniani (IMF) lilisema kwamba wakati Tanzania "ikiwa katika hatari kubwa zaidi ya kuathirika na mabadiliko ya tabianchi", nchi hiyo haikuwa "imejiandaa kuliko nchi nyingi kukabiliana na maafa."

Mnamo Januari 24, kampuni ya East African Crude Oil Pipeline (EACOP) Ltd, ambayo shughuli zake ni kuchimba mafuta ya ardhini, ilipata leseni iliyoiruhusu kuanza ujenzi wa kilomita 1,443 za Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kusafirisha mafuta kutoka visima vya mafuta vya Ziwa Albert magharibi mwa Uganda kwenda bandari ya Tanga kwenye pwani ya kaskazini mwa Tanzania kwa ajili ya kuuza nchi za nje (angalia ripoti ya Uganda). Mradi huu unahusisha ujenzi wa bomba linalopashwa joto lenye kipenyo cha sentimita 61.

Mnamo Aprili 5, Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki (EACJ) iliahirisha kutoa hukumu katika kesi iliyofunguliwa miaka mitatu nyuma na asasi za kijamii za Kenya, Uganda na Tanzania zilizotaka kuwekwa zuio la muda kwa lengo la kuzuia ujenzi wa bomba hilo. Mahakama ya EACJ ilisikiliza hoja kutoka kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, na serikali za Tanzania na Uganda ambazo zilitoa hoja moja, kati ya nyingi, kwamba kesi hiyo ilikuwa nje ya mamlaka ya mahakama hiyo kuisikiliza. Asasi za kiraia zilikuwa zimefungua kesi kutokana na hofu ya madhara makubwa ya ujenzi wa bomba hilo kwenye mazingira na uhamishaji wa watu wa eneo hilo, wakiwemo Wakazi wa Asili, ambao haki yao ya kupata mahitaji muhimu, chakula na afya ilihatarishwa na mradi huo. Mnamo Novemba 29 mahakama ilitupilia mbali kesi hiyo ya madai kwa kuwa ilifunguliwa nje ya muda ikitoa uamuzi kwamba walalamikaji walipaswa kufungua kesi hiyo mapema mwaka 2017 badala ya mwaka 2020. Asasi za kijamii zilikata rufani dhidi ya uamuzi huu mnamo Desemba 11.

## HAKI YA KUPATA UKWELI, HAKI NA FIDIA

Serikali ilikanusha taarifa zilizoenea kuhusu vitendo vya ukatili wakati wa zoezi la kuwahamisha kwa nguvu Wamaasai kutoka ardhi yao huko Ngorongoro. Pia ilikataa maombi kutoka mashirika ya kimataifa kufanya ziara za kutafuta ukweli huko Ngorongoro. Serikali hata hivyo, iliruhusu ujumbe wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kufanya ziara ya uhamasishaji kati ya Januari 23 na 28. Ujumbe huo ulitoa dukuduku kuhusu kuwahamisha kwa nguvu Wamaasai, ukizingatia kutokuwepo ushauriano wa kutosha, na uhusishwaji wa jamii katika zoezi la kuweka mipaka kwenye ardhi wanayodai ni yao; na taarifa za matumizi ya nguvu na vitisho dhidi ya wanajumuiya waliopinga zoezi la uwekaji mipaka. Mnamo Agosti 25, serikali ilizuia ujumbe wa UNESCO wa kutafuta ukweli, kutembelea eneo hilo. Kwa mara nyingine tena, ujumbe wa Bunge la Ulaya ulikataliwa kwenda, licha ya serikali hapo awali kukubali ziara yao kwenda kuchunguza suala la ukiukwaji wa haki za Wamaasai.

Matangazo ya serikali yaliyotolewa mwaka 2022 yakionesha kwamba itapitia upya uamuzi wake wa kuondoa tamko lililowekwachini ya Kanuni ya 34(6) ya Itifaki ya Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR), haukuwa umetekelezwa. Hivyo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) na watu binafsi ambao waliona hawakutendewa haki na mfumo wa sheria wa nchi, waliendelea kukosa uwezo wa kutumia moja kwa moja mahakama ya AfCHPR. Serikali ilikuwa imeandika kusudio la kujiondoa mwaka 2019.

## HAKI ZA WANAWAKE NA WASICHANA

Utafiti wa Kufuatilia Kaya Tanzania (NPS) ulionesha kwamba ingawa kulikuwa na maendeleo katika utoaji wa elimu bora, bado kulikuwa na haja ya kufanya maboresho hususan kuhusu idadi ndogo ya wasichana kuendelea na masomo. Licha ya kwamba mnamo Februari 2022 liliondolewa katazo lililodumu miaka mitatu la wasichana wanaopata mimba na akina mama vijana kutoendelea na masomo, bado kulikuwa na idadi ndogo ya wanaoendelea na masomo kutokana na umaskini, mimba za utotoni na ukatili wa kijinsia mashuleni. Hata hivyo kulikuwa na ongezeko la jumla la watoto kuandikishwa shule na viwango vya ufahamu wa kusoma na kuandika, na upunguaji wa vizuizi vinavyokwamisha watoto kwenda shule. Ripoti ya Benki ya Dunia ilihitimisha kwamba "sera na mikakati ya serikali … iliwezesha nchi kuelekea hatua ya watoto wengi zaidi kupata elimu, hasa katika maeneo yenye huduma duni."

## HAKI ZA WAPENZI WA JINSIA MOJA (LGBTI)

Mwezi Februari, Waziri wa Elimu alipiga marufuku matumizi ya vitabu katika shule za serikali na za binafsi vyenye maudhui ya LGBTI, na kuomba umma kutoa taarifa ya vitabu vyovyote vyenye maudhui kama hayo.

Mwezi Machi, mkuu wa jumuiya ya wanawake ya Chadema alitoa wito kwa serikali kutunga sheria ambayo itaruhusu kuhasiwa kwa mtu yoyote atakayetiwa hatiani kufanya mapenzi ya jinsia moja

kwa ridhaa yake. Mnamo Aprili 12, Mbunge mmoja alianzisha mjadala Bungeni, akitoa hoja kwamba kama hatua hazitachukuliwa, Tanzania ilikuwa kwenye “hatari ya kuwa na mashoga katika nafasi za madaraka na mamlaka.” Mbunge mwingine alipendekeza kutumika kwa adhabu ya kifo kwa watu watakaotiwa hatiani kufanya mapenzi ya jinsia moja kwa ridhaa yao.

# HALI YA HAKI ZA BINADAMU DUNIANI

## APRILI 2024

Kila mwaka, Amnesty International inatoa ripoti ya hali ya haki za binadamu duniani. Utafiti wetu unaonesha kwamba, duniani kote, mamlaka zinaendelea kuminya uhuru wa watu. Nchi na makundi yenye silaha yanavunja na kupindisha sheria za vita huku ubaguzi wa rangi ukiwa kiini cha baadhi ya mapigano ya silaha na kujihami baada ya mashambulizi hayo. Migogoro ya kiuchumi, mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira umeathiri jumuiya maskini kwa kiasi kikubwa zaidi. Watetezi wa haki za binadamu wanaoendesha kampeni za haki za jumuiya hizi hushambuliwa kama sehemu ya mpango mkubwa zaidi wa kuzima mawazo tofauti. Mashambulizi yameongezeka zaidi dhidi ya wanawake na wasichana na wapenzi wa jinsia moja (LGBTI). Uhamasishaji wa chuki na machapisho mengine yenye maudhui hatarishi mitandaoni dhidi ya baadhi ya makundi yanayobaguliwa kwa misingi ya rangi yameongezeka. Wakati huo huo, maendeleo makubwa katika teknolojia ya akili bandia (AI) hutumika katika kudhibiti uhuru na kuvunja haki za binadamu.

Hili ni chapisho linalojumuisha Muhtasari wa kanda ya Afrika, na nchi za Kenya na Tanzania kwenye ripoti hiyo ya Amnesty International inayoelezea wasiwasi kuhusu haki za binadamu kwa mwaka 2023 katika nchi 155, ikiunganisha masuala mbalimbali katika ngazi ya kanda na kimataifa na kuangazia ni nini kinachoweza kutokea siku za usoni. Inatoa wito wa nini kifanyike na kuonesha hatua ambazo serikali na wengineo wanaweza kuchukua ili kukabiliana na changamoto hizi na kuboresha maisha ya watu katika nchi hizi mbili za Afrika Mashariki. Ni chapisho muhimu la kusomwa na viongozi wa serikali, watunga sera, watetezi, wanaharakati na mtu yeyote anayevutiwa na haki za binadamu.

**amnesty.org**

AMNESTY INTERNATIONAL